# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.17 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) JULAI 2022

# WALIMU 9,800 WAPANGIWA VITUO VYA KAZI

- Walimu 5000 wapangiwa shule za msingi.
- Walimu 4800 wapangiwa shule za sekondari.
- Walimu 261 wenye ulemavu waajiriwa.










**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# WALIMU WA AJIRA MPYA ZINGATIENI MAADILI YA KAZI YA UALIMU ILI KULINDA AJIRA ZENU

Hivi karibuni Serikali kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) imetangaza walimu waliobahatika kupata ajira katika utumishi wa Umma na kupangiwa kufundisha katika Shule za Msingi na Sekondari kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa mbalimbali hapa nchini.

Waziri Bashungwa alieleza kuwa kwa upande wa kada ya ualimu, waombaji wenye sifa waliokidhi vigezo na kupangiwa vituo vya kazi ni 9,800 ambapo jumla ya walimu 5,000 wamepangwa shule za msingi na walimu 4,800 shule za Sekondari, wakiwemo walimu wenye ulemavu wa shule za msingi na sekondari 261.

Tunasema kuwa kundi hili la walimu 9,800 wamepata bahati kwa sabau idadi hii ni ndogo sana ikilinganishwa na wale wote waliowasilisha maombi ya ajira katika kada hii ya ualimu. Itakumbukwa kuwa jumla ya waombaji kwenye kada ya ualimu walikuwa 123, 390, hivyo, unaweza kuona kuwa walimu ambao hawakubahatika kupangiwa vituo vya kazi ni 113,590.

Tunawapongeza na kuwakaribisha katika utumishi wa umma walimu wapya waliopangiwa vituo vya kazi. Hata hivyo, ni muhimu kwa kila aliyepata fursa hii kutambua kwamba utumishi wa walimu una miiko na maadili yake, hivyo ili kila mmoja kulinda ajira yake, kuzingatia miiko na maadili ya kazi ni jambo lisiloepukika. Vilevile, tukumbuke kuwa kuna kundi kubwa la watu wenye sifa ambao wanatamani kupata nafasi hizo, hivyo yule ambaye hatazingatia taratibu za ajira yake kikamilifu ni rahisi sana kupoteza bahati hiyo aliyoipata.

Tunapokwenda kwenye vituo vyetu vipya vya kazi tuzingatie kuwa wajibu wetu mkubwa ni kumlea mwanafunzi kiroho, kimwili na kiakili. Serikali na jamii kwa ujumla haitarajii kusikia vitendo vya ukiukwaji wa maadali ya ualimu ikiwemu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi, kuadhibu wanafunzi kinyume na utaratibu, kutofundisha darasani, kuchelewa kazini, utoro, kutotii viongozi, kufanya vitendo vinavyodhalilisha utumishi wa umma na matendo mengine ambayo ni kinyume na sheria.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama


**Wajumbe**
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania   tumeyautumishiwawalimutanzania

# WALIMU 9,800 WAPANGIWA VITUO VYA KAZI

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Innocent Bashungwa amesema jumla waombaji wa ajira 9,800 wa Kada ya ualimu wamepangiwa vituo vya kazi kufuatia kibali cha ajira kwa kada za elimu na afya kilichotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan mwezi Aprili, 2022.

Waziri Bashungwa ametoa kauli hiyo hivi karibuni jijini Dodoma alipokutana na waadishi wa habari kutoa taarifa ya kukamilika kwa zoezi la kushughulikia ajira hizo pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali kwa waajiri na waajiriwa wapya.

Alianza kwa kueleza kuwa baada ya kupata kibali cha ajira, ofisi yake ilitoa tangazo kwa wahitimu wa Ualimu na Kada za Afya, kuwasilisha maombi ya kazi kupitia mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kuchakata maombi ya ajira, zoezi ambalo lilifanyika kuanzia Aprili 20 hadi Mei 8, 2022.

"Jumla ya maombi 165,948 yakiwemo ya wanawake 70,780 na wanaume 95,168 yaliyopokelewa kwenye mfumo, ambapo maombi ya kada za afya yalikuwa 42,558, na kada ya Ualimu yalikuwa 123, 390," alisema Waziri Bashungwa.

Alieleza kuwa katika kufanikisha zoezi hilo ofisi yake iliunda timu maalum iliyowahusisha wataalamu kutoa Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTVET), Sekretarieti ya Ajira, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mabaraza ya Kitaalamu katika Sekta ya Afya.

"Timu hiyo ilipewa vigezo vilivyoandaliwa kama mwongozo wa kutoa ajira kwa waombaji, kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa haki na uwazi katika zoezi hilo. Kila kigezo kilichowekwa kilizingatia masuala ya jinsia ili kuhakikisha ajira hizi zinatolewa zinagusa waombaji wa pande zote," alisema Bashungwa.

Akizungumzia matokeo ya kazi hiyo kwa upande wa kada za ualimu, alisema waombaji wenye sifa waliokidhi vigezo na kupangiwa vituo vya kazi ni 9,800 ambapo jumla ya walimu 5,000 wamepangwa Shule za Msingi na






# WALIMU 9,800 WAPANGIWA VITUO VYA KAZI

walimu 4,800 Shule za Sekondari pamoja na walimu 261 wenye ulemavu waliopangiwa shule za msingi na sekondari.

"Katika hao walimu 5000 walipangiwa shule za msingi, wanawake ni 2,353 sawa na asilimia 47.06 na wanaume ni 2,647 sawa na asilimia 52.94. Kwa upande wa walimu 4800 wa shule za sekondari, wanawake ni 1,289 sawa na asilimia 26.85 na wanaume ni 3,511 sawa na asilimia 73.15. Walimu wenye ulemavu 261 wa shule za Msingi na Sekondari walioajiriwa ni sawa na asilimia 2.66 ya walimu wote walioajiriwa ambapo wanawake ni 84 na wanaume ni 177," alisema Waziri Bashungwa.

Kwa upande wa kada za Afya, Waziri Bashungwa alisema waombaji waliokidhi vigezo na kupangiwa vituo vya kazi ni 6,876 ambapo katika idadi hiyo wanawake ni 3,217 sawa na asilimia 46.8 na wanaume ni 3,659 sawa na asilimia 53.2 wakiwemo wenye ulemavu 42 sawa na asilimia 0.61.

Katika hatua nyingine, Waziri bashungwa alitoa maelekezo kwa wajiriwa wapya pamoja na waajiri ambapo alisema waajiriwa wapya wote wahakikishe wanaripoti kwa wakurugenzi wa halmashauri walizopangiwa na kila mmoja awe na Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho ya NIDA, cheti halisi cha kuzaliwa na vyeti halisi vyote vya Taaluma na Utaalamu wa Kazi ili vihakikiwe na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira.

"Waajiri wahakikishe wanapokea vyeti na kuviwasilisha baraza la mitihani kwa ajili ya uhakiki. Wizara ipewe taarifa mara moja kwa wale watakaokutwa na vyeti ambavyo ni vya kughushi ili hatua kali zichukuliwe. Waajiri wahakikishe watumishi wapya waliopangwa kwenye halmashauri, wanapewa barua za ajira, na kuripoti kwenye vituo walivyopangiwa tu, na si vinginevyo," alisema Waziri Bashungwa.

Waziri huyo alionya waajiriwa wenye tabia ya kuchukua posho ya kujikimu na kutokomea kusiko julikana na kusema kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atakayefanya jambo la namna hiyo huku akisisitiza kuwa waajiriwa wapya ambao hawataripoti katika vituo walivyopangiwa katika kipindi cha siku 14, kuanzia tarehe 26 Juni, 2022 watakuwa wamepoteza nafasi zao ambazo zitajazwa na waombaji wengine wenye sifa waliopo kwenye Kanzidata ya ofisi yake.

Pia alitoa maelelekezo kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo Waajiriwa wapya wamepangwa kuhakikisha wanawapokea na kuwawezesha kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma, na kuwasilisha kwake taarifa ya zoezi hilo kupitia mfumo wa kielektroniki (ajira.tamisemi.go.tz), kila mtumishi anapopokelewa na kukamilisha taratibu za ajira.



# RAIS SAMIA AENDELEA KUIMARISHA SEKTA YA ELIMU, AFUTA ADA KIDATO CHA TANO NA SITA

**Na Mwandishi Wetu – Dodoma.**



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Shuluhu Hassan ameendeleza jitihada zake za kuboresha sekta ya elimu nchini na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi mwenye sifa za kupata elimu anatimiza ndoto zake bila kipingamizi chochote.

Safari hii jitihada za Rais Samia zimeonekana tena kwa kuamua kufutwa ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita ili kuwapunguzia gharama wazazi na walezi na kusaidia wanafunzi wengi hasa wale ambao familia zao zina kipato kidogo, kupata fursa ya kusoma bila vikwazo.

Habari njema hizo zilitolewa hivi karibuni na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Mwigulu Nchemba




*Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akionesha Mkoba wa Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka 2022/23 alipowasili katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma hivi karibuni.*

bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023 ambapo alisema wanafunzi wa kidato cha tano ni takribani 90,825 na kidato cha sita ni 56,880 na mahitaji ya fedha ni Sh10 3 bilioni.

"Mheshimiwa Spika, kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni takriban 90,825 na kidato cha sita ni 56,880. Mahitaji ya fedha ni shilingi 10,339,350,000. Ili kuwapunguzia gharama watoto hao kama Mheshimiwa Rais alivyoielekeza Wizara, napendekeza kufuta ADA kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Kwa hatua hiyo, Elimu bila Ada ni kuanzia shule za msingi mpaka kidato cha sita. Serikali itajipanga kuangalia namna ya kusaidia vyuo vya kati kadiri hali ya uchumi itakavyotengemaa," alisema Waziri huyo.

Nao wabunge walionekana kupokea mapendekezo hayo na kuyakubali kwa kile kinachoonekana kuwa utekelezwaji wa zoezi hilo unakwenda kuwapunguzia wananchi mzigo wa gharama na hivyo kuendelea kuboresha maisha yao.



*Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2022/23, bungeni, jijini Dodoma hivi karibuni.*

# KUTOZINGATIWA KWA MAADILI YA KAZI YA UALIMU KUNAPUNGUZA TIJA YA UTOAJI WA ELIMU BORA NCHINI: NKWAMA



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama.*

**Na Mwandishi Wetu – Tabora.**

Maadili ya kazi ya Ualimu ni Utaratibu au Mwongozo uliokubalika kuhusu Mwenendo, Tabia na Imani ya mtu afanyaye kazi ya kufundisha watoto/wanafunzi, kuangalia afya na ukuaji wao kitabia na kimaadili wawapo shuleni na hata nje ya shule. Miiko ya Ualimu ni mambo ambayo Mwalimu hatakiwi kuyafanya kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Kazi ya ualimu inapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia miiko na maadili yake ili iendelee kuandaa rasilimaliwatu wenye ujuzi, maarifa, weledi, wachapakazi na wazalendo kwa nchi. Wataalam wa fani zote hupita kwenye mikono ya Walimu. Hivyo walimu wenye maadili na wanaozingatia miiko husababisha matokeo chanya kwa wanafunzi na hatimaye kujenga Taifa lenye amani, utulivu, watu waadilifu na maendeleo.

Kutozingatiwa kwa Maadili ya kazi ya Ualimu kumesababisha walimu kutenda makosa mbalimbali ambayo hupunguza tija ya utoaji elimu bora nchini. Katika Kipindi cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2020/21 jumla ya makosa 10,835 yayojitokeza kutendwa mara kwa mara na walimu ambapo asilimia 68 ya walimu waliotenda makosa hayo walipewa adhabu ya kufukuzwa kazi.

Miongoni mwa makosa yaliyoonekana kutendwa mara kwa mara na idadi yake ambayo imewekwa kwenye mabano ni; utoro (6,709), kukiuka maadili ya kazi ya ualimu (1,500), kughushi (1,353), mahusiano ya kimapenzi na wanafuzi (554), ulevi (230), ukaidi na kutotii (395) na uzembe kazini (94).

Hayo yamebainishwa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama wakati akitoa wasilisho la mada juu ya masuala ya Utumishi wa Walimu katika Mkutano wa Maafisa Elimu wa Mikoa uliofanyika mjini Tabora hivi karibuni.

Nkwama amesema ili kukabiliana na changamoto za walimu kukiuka maadili ya taalauma yao TSC imejipanga kutoa mafunzo kwa walimu hususani wanapoanza utumishi wao ili waelewe kwa undani kuhusiana na maadili ya kazi hiyo na kuweza kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuwaingiza katika kutenda makosa.

Nkwama aliongeza kuwa TSC inaona kuna haja kwa walimu kupatiwa ushauri nasaha na unasihi kwa kuwa baadhi yao wanajikuta wameingia kwenye makosa ya kinidhamu kutokana msongo wa mawazo unaosababisha mwalimu kushindwa kufanya maamuzi sahihi.

Katibu aliendelea kueleza kuwa moja ya mambo yanayosaidia walimu kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia miiko na maadili ya kazi ni kupatiwa motisha jambo ambalo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amelipatia kipaumbele kwa kuwapandisha madaraja pamoja na kuridhia nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma.

Pamoja na njia hizo, kiongozi Nkwama alisema kuwa njia nyingine ya kumaliza changamoto ya walimu kukikuka maadili ya kazi yao ni TSC kuendelea kuchukua hatua za kinidhamu na kutoa adhabu kwa walimu watovu wa nidhamu ili iwe fundisho kwao, walimu wenzao na jamii kwa ujumla.




Picha ya marehemu Yohana Peter Mpande wakati wa uhai wake.



Picha ya marehemu Yohana Peter Mpande wakati wa uhai wake.



Watumishi wa TSC wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa marehemu Yohana Peter Mpande wakati wa hafla ya kuaga mwili marehemu Mpande iliyofanyika nyumbani kwa marehemu huyo Ihumwa jijini Dodoma Juni 24, 2022.




Jeneza lenye mwili wa Marehemu Yohana Peter Mpande likiingizwa nyumbani kwa marehemu huyo eneo la Ihumwa jijini Dodoma wakati wa hafla ya kuaga mwili marehemu Mpande iliyofanyika Juni 24, 2022.



Mwenyekiti wa TSC, Prof. Lazaro Komba akitoa salamu za rambirambi wakati wa hafla ya kuaga mwili wa Marehemu Yohana Peter Mpande iliyofanyika nyumbani kwa marehemu eneo la Ihumwa jijini Dodoma Juni 24, 2022.



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akitoa salamu za rambirambi wakati wa hafla ya kuaga mwili wa Marehemu Yohana Peter Mpande iliyofanyika nyumbani kwa marehemu eneo la Ihumwa jijini Dodoma Juni 24, 2022.*



*Mtumishi wa TSC, Charles Novat akisoma wasifu wa Marehemu Yohana Peter Mpande wakati wa hafla ya kuaga mwili wa marehemu huyo iliyofanyika nyumbani kwa marehemu eneo la Ihumwa jijini Dodoma, Juni 24 2022.*



*Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akitoa salamu za rambirambi wakati wa hafla ya kuaga mwili wa Marehemu Yohana Peter Mpande iliyofanyika nyumbani kwa marehemu eneo la Ihumwa jijini Dodoma Juni 24, 2022.*



*Mwakilishi wa familia ya marehemu Yohana Peter Mpande akitoa shukrani wakati wa hafla ya kuaga mwili wa Marehemu Yohana Peter Mpande iliyofanyika nyumbani kwa marehemu eneo la Ihumwa jijini Dodoma Juni 24, 2022.*

*Mwakilishi kutoka iliyokuwa Ofisi ya Rais Tume ya Mipango ambapo marehemu Yohana Peter Mpande aliwahi kufanya kazi akitoa salamu za rambirambi wakati wa hafla ya kuaga mwili wa marehemu iliyofanyika nyumbani kwa marehemu eneo la Ihumwa jijini Dodoma Juni 24, 2022.*



# BURIANI YOHANA PETER MPANDE



*Waombolezaji waliohudhuria msiba wa marehemu Yohana Peter Mpande. Msiba huo ulifanyika nyumbani kwa marehemu Mpande eneo la Ihumwa jijini Dodoma.*

**Na Mwandishi wetu - Dodoma**

Simanzi na vilio vimetanda Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kufuatia kifo cha Mtumishi wa TSC Makao Makuu, Bw. Yohana Peter Mpande ambaye alikuwa Afisa Ukaguzi Mwandamizi aliyefariki dunia tarehe 22/06/2022 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma alipokuwa akipatiwa matibabu.

Akitoa Salamu za pole wakati wa kuaga mwili wa Marehemu, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alieleza kuwa alipokea taarifa za kifo cha mtumishi huyo kwa mstuko mkubwa huku akieleza namna mtumishi huyo alivyomfahamu wakati wa uhai wake.

"Taarifa za kifo cha ndugu yetu zilinistua sana, binafsi nilikuwa namfamu vizuri marehemu, alikuwa mpole, mcheshi na mchapakazi hodari. Sikuwahi kujua kuwa marehemu alikuwa anapambana na maradhi kwa muda mrefu, kila wakati tulipokutana alikuwa mwenye tabasamu, mkakamavu na hakujionesha kama alikuwa na tatizo la kumfanya ashindwe kutekeleza majukumu yake."

"Najua sote tuna majonzi sana kwa kumpoteza ndugu yetu huyu lakini tunachoweza kujifunza hapa ni kwamba kila mmoja wetu ajitahidi kutenda mema kwa kuwa hakuna anayejua zamu yake ya kuondoka hapa duniani ni lini. Tufanye kazi tulizopewa kwa bidii, weledi na maarifa huku tukidumisha umoja, upendo na ushirikiano kwa kuwa kila mmoja ataondoka kwa wakati waki na kifo hakitoi taarifa," alisema Prof. Komba.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alisema kuwa Marehemu Mpande alikuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa





*Waombolezaji waliohudhuria msiba wa marehemu Yohana Peter Mpande. Msiba huo ulifanyika nyumbani kwa marehemu Mpande eneo la Ihumwa jijini Dodoma.*

# BURIANI YOHANA PETER MPANDE



*Waombolezaji waliohudhuria msiba wa marehemu Yohana Peter Mpande. Msiba huo ulifanyika nyumbani kwa marehemu Mpande eneo la Ihumwa jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa Marehemu Yohana Peter Mpande Juni 24, 2022 jijini Dodoma.*

Shinikizo la Damu kwa muda mrefu na alikuwa akipatiwa matibabu katika hospitali mbalimbali ikiwemo hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.

Alifafanua kuwa kutokana na tatizo hilo kuendelea kumsumbua, ofisi yake ilianza taratibu za kumsaidia mtumishi huyo ili aweze kupata uhamisho wa kwenda katika eneo ambalo lingekuwa rafiki zaidi kulingana na afya yake.

"Wakati tukiendelea na taratibu za kushughulikia uhamisho wake, tarehe 17 Juni, 2022 akiwa anatoka kazini, marehemu alijisikia vibaya na kukimbizwa katika zahanati ya Makole kwa matibabu. Hali yake iliendelea kuwa mbaya na hivyo akapewa rufaa kwenda Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu zaidi ambapo alipatiwa matibabu chini ya uangaizi maalum kwa muda wa siku tano hadi umauti ulipomfika tarehe 22 Juni, 2022 saa 4:50 asubuhi," alisema Nkwama.

Katibu huyo alieleza kuwa, Marehemu Mpande alikuwa mfanyakazi mzuri ambaye licha ya changamoto za ugonjwa alizokuwa nazo, aliendelea kutekeleza majukumu yake ya ukaguzi kwa bidii, weledi na uzalendo na kuifanya TSC kuendelea kuwa na matumizi mazuri ya rasilimali za Serikali.

"Mwaka 2018 Mpande alipohamia TSC alikuwa mtumishi pekee katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na kwa zaidi ya mwaka mmoja alifanya kazi akiwa peke yake kwenye Kitengo. Kwa kweli amekuwa akitoa ushauri chanya kwa Taasisi na kuisaidia Tume kuendelea kupiga hatua zaidi katika kutekeleza majukumu yake," alisema.

Alimalizia kwa kusema, "tunatoa pole sana kwa ndugu



*Katibu wa TSC, Prof. Paulina Nkwama akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa Marehemu Yohana Peter Mpande Juni 24, 2022 jijini Dodoma.*

# BURIANI YOHANA PETER MPANDE



*Jeneza lenye Mwili wa marehemu Yohana Peter Mpande likiwa ndani ya kaburi wakati wa mazishi ya marehemu Mpande yaliyofanyika Juni 25, 2022 Mbarali mkoani Mbeya.*



*Baadhi ya ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Yohana Peter Mpande wakipiga picha ya kumbukumbu kwenye kaburi la marehemu Mpande mara baada ya kumalizika kwa shughuli za mazishi zilizofanyika Mbarali mkoani Mbeya, Juni 25, 2022.*

jamaana marafki wa familia ya Mpendwa wetu, Yohana Mpande. Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Madaktari na Wauguzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kwa jitihada walizofanya ili kuokoa maisha ya mpendwa wetu. Pia tunawashukuru ndugu, jamaa, marafiki na majirani wa marehemu kwa ushirikiano wao tangu kipindi cha kuugua hata sasa tunapoelekea kumpumzisha mpendwa wetu."

Kwa mujibu wa wasifu wa marehemu, Bw. Yohana Peter Mpande alizaliwa tarehe 5/3/1969 katika Kijiji cha Ihahi Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya akiwa mototo wa nne katika familia ya Marehemu Mwalimu Peter Mpande na Bi. Anna Mlawa.

Marehemu Mpande alipata elimu yake ya msingi katika shule ya Msingi Isitu iliyopo Chimala Mbeya mwaka 1979 na kuhitimu mwaka 1985 na mwaka 1986 alijiunga na elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari Iyunga Mbeya ambapo alihitimu kidato cha nne mwaka 1989 huku akipata elimu ya kidato cha Tano na Sita mwaka 1990 hadi 1992 katika shule ya Sekondari Tosamaganga iliyopo mkoani Iringa.

Mwaka 1993 Marehemu alihitimu mafunzo ya Askari Magereza katika Chuo cha Magereza Kiwia kilichopo mkoani Mbeya na mwaka 1997 hadi 1998 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kutunukiwa Astashahada ya Sheria kabla ya kujiunga na Chuo cha Uhasibu (TIA) kilichopo Kurasini jijini Dar es Salaam mwaka 2001 ambapo alitunukiwa Stashahada ya Juu ya Uhasibu na mwaka 2010 hadi 2012 alijiunga na Chuo Kikuu cha Coventry cha nchini Uingereza na kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Fedha na Uwekezaji.

Marehemu Mpande aliajiriwa na Wizara ya Mambo ya Ndani kama Askari Magereza amapo alipangiwa kufanya kazi katika gereza la Maweni mkoani Tanga kuanzia mwaka 1994 hadi mwaka 2004, mwaka 2005 hadi 2009 aliajiriwa na Kampuni ya Kilicafe Mbeya katika nafasi ya Uhasibu, mwaka 2009 aliajiriwa na iliyokuwa Ofisi ya Rais, Tume ya Taifa ya Mipango akiwa Mkaguzi wa Ndani na mwaka 2018 alijiunga na Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Walimu ambapo aliendelea kufanya kazi akiwa Afisa Ukaguzi wa Ndani Mwandamizi hadi umauti ulipomkuta.

Baada ya kumalizika shughuli za kuaga mwili wa marehemu jijini Dodoma, safari ya kuelekea Mkoani Mbeya kwa ajili ya mazishi ilianza ambapo Juni 25, 2022 mazishi ya marehemu Yohana Peter Mpande yalifanyika huko Mbarali Mbeya.

# TANZIA



**(1969 – 2022)**

Uongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), unasikitika kutoa taarifa ya kifo cha Mtumishi mwenzetu,

**Ndg. Yohana Peter Mpande - Afisa Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali**

Kilichotokea Asubuhi ya Siku ya Jumatano Juni 22, 2022 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma akipatiwa matibabu na kuzikwa Siku ya Jumamosi Juni 25, 2022 Wilayani Mbarali, Mkoani Mbeya.

*"Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe na Apumnzike kwa Amani, AMINA."*


OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)
TANZANIA
SENSA
23 Agosti
2022
Jiandae Kuhesabiwa
16
JUNI
Tunakutakia Kheri katika
Maadhimisho ya siku ya
MTOTO WA AFRIKA


16
JUNI
Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)
Mwl. Paulina M. Nkwama, *ndc* anawatakia
Maadhimisho mema ya siku ya Mtoto wa
AFRIKA
Tuimarishe ulinzi wa Mtoto, Tokomeza Ukatili dhidi yake. Jiandae Kuhesabiwa”

# MWALUSAMBA ATETEA NAFASI YA UENYEKITI, UCHAGUZI MKUU WA SHIMIWI



*Mwenyekiti wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Daniel Mwalusamba akila kiapo baada ya kuchaguliwa tena na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa shirikisho hilo kwa kura 70 kati ya 100 uliofanyika leo kwenye ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Mount Uluguru, mkoani Morogoro.*



*Msimamizi wa uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Leonard Thadeo (aliyenyoosha kidole) wakati akizungumza na wajumbe waliokasimiwa madaraka na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kusimamia uchaguzi huo wakiwa wanazungumza mambo mbalimbali baada ya zoezi hilo kukamilika kwenye ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Mounti Uluguru, mkoani Morogoro.*

**Na. Mwandishi Wetu – Morogoro.**

WAJUMBE 70 kati ya 100 wa mkutano mkuu wa uchaguzi wamemchagua Daniel Mwalusamba kuwa Mwenyekiti wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), katika uchaguzi uliofanyika leo kwenye ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Mount Uluguru, mkoa wa Morogoro.

Msimamizi wa uchaguzi huo uliosimamiwa kwa umahiri mkubwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leonard Thadeo alisema nafasi hiyo iliwaniwa na wanamichezo wawili, ambapo Eliud Mwaiteleke alipata kura 30; huku nafasi ya Makamu



*Mmoja wa wajumbe wa uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Mohamed Ally (wapili kulia) akisimamia zoezi la kuhesabu kura za wagombea wa nafasi ya ujumbe wa kamati ya utendaji katika uchaguzi uliofanyika leo kwenye ukumbi wa Hoteli ya Mount Uluguru, mkoani Morogoro.*

# MWALUSAMBA ATETEA NAFASI YA UENYEKITI, UCHAGUZI MKUU WA SHIMIWI

Mwenyekiti ikichukuliwa na Alquine Masubo aliyepata kura 64 na kuwashinda Kaundime Kizaba mwenye kura 18 na Chilemba Chikawe kura16.

Thadeo alisema Alex Temba amechaguliwa kwa kura 80 kuwa Katibu Mkuu na kumshinda Mussa James mwenye kura 20; na Katibu Msaidizi alichaguliwa Mariam Kihange aliyepata kura 56 na kuwashinda Mfaume Mfaume (21), Andrew Sekimweri (14) na Mwinjuma Bwanga (7); na huku Rose Makange aliyekuwa hana mshindani ameshinda kwa kishindo nafasi ya Uweka Hazina Mkuu kwa kuzoa kura zote 100.

Wajumbe wawili wa Viti Maalum wanawake wameshinda Itika Mwankenja kwa kura 81 na Bahati Mollel kwa kura 68, huku Assumpta Mwilanga alishindwa kwa kupata kura 37; na wajumbe watano wa Kamati ya Utendaji walioshinda ni Tumsifu Mwasamale (91), William Moye (89), Apolinary Kayungi (85), Damian Manembe (83) na Mashaka Mwamage (74), huku Fidelis Choka (57) alishindwa.

Hatahivyo, Thadeo amesema wanamicbezo 21 ndio waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali, huku wapiga kura walikuwa 100, ambapo amewashukuru wagombea wote kwa kushiriki vyema hatua zote ikiwemo ya awali ya usaili na baadaye uchaguzi bila ya kuwa na matatizo, hali kadhalika kwa wapiga kura nao kufuata taratibu na kanuni zilizokuwa zimewekwa na BMT na kufanikisha uchaguzi huo salama.

"Wanamichezo wameitikia wito na kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali tangu ilivyotangazwa hata kwenye usaili walioweza kufika ni 16 baada ya watano kushindwa kufika na ndio waliochujwa, na kimsingi uchaguzi ulikwenda vizuri sana maana tulipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wenzetu na pia hatujapata malalamiko kutoka kwa wagombea walioshindwa," amesema Thadeo.

Naye Mwalusamba aliwashukuru wajumbe kwa kumchagua tena katika nafasi ya Uenyekiti kwa kuwa wameonesha imani kubwa katika utendaji wake wa kazi na kumpa dhamana ya miaka minne tena ya kuongoza, ambapo ameahidi kwa kushirikiana na viongozi wenzake wa kamati ya utendaji watahakikisha wanatekeleza maazimio yote waliyojiwekea kwenye mkutano mkuu.



*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), wakifurahia jambo wakati wa mchakato wa upigaji kura uliofanyika leo kwenye ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Mount Uluguru,, mkoani Morogoro.*



*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), wakifuatilia kwa makini masuala yaliyokuwa yakielezwa na msimamizi wa uchaguzi huo, Leonard Thadei (hayupo pichani) kwenye ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Mount Uluguru,, mkoani Morogoro.*

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS
## TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

# MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA 16 - 23 JUNI 2022



Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**KAULI MBIU**

"Nafasi ya Mapinduzi ya nne ya Viwanda katika masuala mapya yanayojitokeza kuhusu utoaji wa huduma na urejeshaji wakati na baada ya janga la Corona"

***Karibu tukuhudumie***

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

---

## OFISI YA RAIS
## TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)



TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

# Wiki ya Utumishi wa UMMA
**17- 23 Juni, 2022**

"Katika Kuadhimisha wiki hii ya Utumishi wa Umma napenda kuwakumbusha Walimu wote kuendelea kufanya kazi zao kwa bidii, uadilifu na kwa kufuata kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma".

Mwl.Paulina M. Nkwama, ndc
Katibu, Ofisi ya Rais - TSC

## Kauli Mbiu

*"Uhusiano kati ya uwezeshaji wa vijana na usimamizi wa masuala ya uhamiaji: Kujenga utamaduni wa usimamizi Utawala Bora, matumizi ya TEHAMA na ubunifu katika utoaji wa Huduma Jumuishi."*

Tume ya Utumishi wa Walimu
www.tsc.go.tz

# TSC YANUFAIKA KUSHIRIKI MKUTANO WA WATAYARISHAJI WA VIPINDI VYA ELIMU KWA UMMA KUPITIA REDIO NA RUNINGA

**Na Mwandishi Wetu – Iringa.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeshiriki mkutano wa 106 wa watayarishaji wa vipindi vya Elimu kwa Umma kupitia redio na runinga ambao uliandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania – TBC na kufanyika kwa siku tano, tarehe 06 – 10 Juni, 2022 mjini Iringa.

Mkutano huo uliwashirikisha Maafisa Habari, Mawasiliano, Itifaki na Uhusiano wa Wizara, Mikoa, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Majiji, Miji na Halmashauri za Wilaya pamoja na wadau wengine kutoka Sekta binafsi.

Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kutoa fursa kwa wadau wa habari kubadilishana uzoefu na kujadili mbinu mbalimbali za kutoa habari kupitia vipindi vya redio na runinga kuhusu kazi zinazofanywa na taasisi zao ili kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya hatua mbalimbali za maendeleo zinazofanyika.

TSC iliwakilishwa na Maafisa wawili kutoka Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali ambao ni ndugu Gerard Chami ambaye ni Mkuu wa Kitengo hicho na ndugu Adili Mhina ambaye ni Afisa Habari.

Taarifa liliyoandaliwa na washiriki hao kutoka TSC ilieleza

> **“TSC ilieleza kuwa mkutano huo ulikuwa na faida kubwa kwa watumishi hao kwani umeendelea kuwaimarisha kiutendaji kitu ambacho kitaongeza ufanisi wa kazi na kuisaidia TSC kupiga hatua zaidi katika kutoa huduma kwa walimu”.**

kuwa mkutano huo ulikuwa na faida kubwa kwa watumishi hao kwani umeendelea kuwaimarisha kiutendaji kitu ambacho kitaongeza ufanisi wa kazi na kuisaidia TSC kupiga hatua zaidi katika kutoa huduma kwa walimu.

“Katika Mkutano huo tulipata fursa ya kujikumbusha mambo mbalimbali yanayohusu namna bora ya kutekeleza majukumu yetu katika nyanja mbalimbali za mawasiliano. Kupitia mada zilizowasilishwa tulijifunza namna tunavyoweza kuandaa vipindi vyenye ubora na mvuto zaidi kwa wadau wetu,” ailisema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza miongoni mwa mambo wawakilishi hao waliojifunza kuwa ni namna bora ya kuandaa bangokitita yenye taarifa muhimu za kuwapatia waandishi wa habari pamoja na namna bora ya kuandaa taarifa inayomrahisishia mwandishi wa habari kupata maudhui na habari iliyokusudiwa.

Faida nyingine iliyopatikana ni kujifunza namna ya kuandaa mkutano wa waandishi wa habari (press conference) kwa kuzingatia siku na muda unaowawezesha waandishi kuandandaa habari na kuziwasilisha kwenye vyombo vyao vya habari na hatimaye ziweze kuwafikia wananchi kwa wakati uliokusudiwa.

Washiriki hao walijifunza pia kuongeza ubunifu na thamani katika maudhui na muonekano wa mitandao ya kijamii, namna bora ya kutumia vyombo vya habari katika kudumisha amani ndani ya jamii na Taifa kwa ujumla na matumizi sahihi ya Lugha ya Kiswahili katika vyombo vya habari.

Taarifa hiyo ilieleza faida nyingine ziliyopatikana kwa kushiriki mkutano huo kuwa ni kujifunza namna ya kuandaa Mpango Mkakati wa Mawasiliano katika utekelezaji, usimamizi na tathmini kwenye miradi ya Serikali pamoja na namna ya kuandaa makala za redio na runinga kwa kuzingatia muundo wa kitaalamu (wazo, utafiti, mpango kazi, uandishi wa muswada, kupiga picha/ kurekodi pamoja na kuhariri makala).

# KATA YA IPAGALA YAWAPONGEZA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI



*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka akiongea wakati wa hafla ya kuwapongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali pamoja na wanafunzi kutoka Kata ya Ipagala jijini Dodoma iliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali pamoja na wanafunzi kutoka Kata ya Ipagala jijini Dodoma wamepongezwa kwenye hafla iliyoandaliwa na Diwani wa Kata hiyo Bw. Gombo Kamuli Doto na kuhudhuriwa na Naibu Waziri - Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Jabir Shekimweri na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde.

Hafla hiyo ilifanyika Juni 28, 2022 katika viwanja vya Shule ya Msingi Mtemi Mazengo ambayo ni moja kati ya shule tano za Msingi za mfano nchini Tanzania.

Akielezea Shule hiyo Bw. Gombo amesema kuwa Shule ya Msingi Mtemi Mazengo ni moja kati ya shule 5 za majaribio zilizojengwa na Serikali kwa lengo la kupima ufaulu kulinganisha na ule wa shule binafsi ambapo shule ina Madarasa 17, Miundo mbinu ya umeme na maji, maktaba, nyumba za walimu 4, ukumbi wa mkutano, viti na meza nzuri za kukalia waalimu pamoja na wanafunzi.

"Ujenzi wa shule hii umegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 1 ambao kati ya hizo Tsh.700 milioni zilitolewa na Serikali Kuu wakati zilizobakia zilitokana na mapato ya ndani. Shule ya Mteni Mazengo imehitimisha darasa la Saba la kwanza mwaka 2021 kwa kuwa na wahitimu 84 ambao wote walifaulu kwa viwango vya juu," alisema Gombo.

Aliendelea kueleza kuwa Kata ya Ipagala ina shule Sita za Serikali huku 4 zikiwa shule za msingi na 2 shule za sekondari (shule ya sekondari Makole na shule ya sekondari Meria). Shule za Msingi zina jumla ya wanafunzi 3190 ambao wote wamefanya vizuri kimkoa na Kitaifa katika matokeo ya Mitihani ya Darasa la Nne na darasa la Saba mwaka 2021.



*Baadhi ya walimu na wazazi waliohudhuria hafla ya kuwapongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali pamoja na wanafunzi kutoka Kata ya Ipagala jijini Dodoma.*

# KATA YA IPAGALA YAWAPONGEZA WALIMU WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Akizungumza, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alimpongeza Diwani wa Kata hiyo huku akiwaasa wazazi kuwa na muda wa kuongea na watoto wao na kuwasaidia ili kuongeza hamasa kwa wanaafunzi kufanya vizuri zaidi katika masomo yao.

Kiongozi huyo ameonesha kuridhishwa na maendeleo ya shule hiyo na kuahidi kuupeleka Mwenge wa uhuru katika shule hiyo mara utakapo tembelea Mkoa wa Dodoma.

"Nichukue fursa hii kuwafahamisha kuwa hiki ni deni kwangu Mwenge utakapokuja MNkoa wa Dodoma basi nitahakikisha utatenmbelea shule ya Msingi Mtemi Mazengo," Amesema Shekimweri.

Nae, Mbunge wa Dodoma Mjini, Mhe. Anthony Mavunde, amempongeza Diwani Gombo, kwa kuwathamini na kuwatambua waalimu, kwani hiyo imekuwa chachu katika utendaji kazi wao, pia imewafanya wanafunzi kuzingatia masomo na kufaulu kiasi cha kutoa mwanafunzi wa kwanza katika mashindano yaliyohusisha shule binanfsi. Aidha Mhe. Mavunde amepongeza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Mtaka kwa kuyapa kipaumbele masuala ya elimu.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Anthony Mtaka, ametoa maelekezo kwa shule zote za Serikali Mkoani Dodoma na kuziagiza kuandaa vikao vya wazazi kila muhula, pindi shule zinapofungwa ili kujadili maendeleo ya Elimu kwa watoto wao kwa kuwa malezi ya watoto ni baina ya mzazi, mwalimu na mtoto mwenyewe, kwani matokeo yakiwa mazuri, pongezi huenda kwa wote hivyo wazazi wawajibike kwa watoto wao.

Nae, Mgeni rasmi Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga alisema kuwa suala la elimu ni la lazima na si hiyari ndio maana Serikali inatimiza wajibu wa kutengeneza miundombinu Bora ya kufundishia kwani Taifa Bora ni lile lenye watu wenye elimu.

"Serikali kwa kutambua umuhimu wa elimu kwenye Mkoa wa Dodoma ambao ndio makao makuu ya nchi, imetoa Shilingi Bilioni 17 kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo kikubwa cha Tehama katika eneo la Nala ambacho tayari kimeanza kujengwa," alisema Kipanga.





*Baadhi ya wanafunzi waliohudhuria hafla ya kuwapongeza Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali pamoja na wanafunzi kutoka Kata ya Ipagala jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga akitoa maelezo kwa wateja waliofika TSC wakati wa Wiki ya Utumishi wa Umma iliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*



*Mteja akiuliza swali kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Kahama, viongozi wa Chama cha Walimu pamoja na wadau wengine wa elimu katika Wilaya hiyo wakiwa katika Mkutano na Waalimu wilayani hapo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*



*Baadhi ya Walimu wilayani Kahama wakiwa katika mkutano ulioongozwa na ofisi ya TSC Wilaya ya Kahama ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*





*Baadhi ya Walimu wilayani Kahama wakiwa katika mkutano ulioongozwa na ofisi ya TSC Wilaya ya Kahama ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*

# TSC YAADHIMISHA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA KWA KUENDELEA KUWAFIKIA WADAU WAKE

**Na Mwandishi wetu.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeungana na taasisi zingine za umma katika kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma ambapo maadhimisho hayo yamefanyika Juni 16 – 23, 2022.

Maadhimisho ya mwaka huu yalibeba kaulimbiu isemayo nafasi ya nne ya mapinduzi ya viwanda katika masuala mapya yanayojitokeza kuhusu utoaji wa huduma na urejeshwaji wakati na baadaya ya janga la Corona.

Kwa upande wa TSC Makao Makuu, maadhimisho hayo yalifanyika kwa kwa kutenga sehemu maalumu ambapo wateja walifika na kupatiwa huduma mabalimbali zikiwemo zinazohusiana na rufaa za walimu, upandishaji vyeo, taarifa za kiutumishi kwa ajili ya maandalizi ya kustaafu (history sheet), kupokea malalamiko na kubadilishiwa cheo/kazi baada ya kujiendeleza kimasomo.

Vilevile baadhi ya Ofisi za TSC ngazi ya wilaya ziliadhimisha wiki ya utumishi wa umma kwa kufanya ziara shuleni nakupata fursa ya kuzungumza na walimu juu ya masuala ya Ajira, Maadili pamoja na maendeleo yao kiutumishi.

**“...baadhi ya Ofisi za TSC ngazi ya wilaya ziliadhimisha wiki ya utumishi wa umma kwa kufanya ziara shuleni nakupata fursa ya kuzungumza na walimu juu ya masuala ya Ajira, Maadili pamoja na maendeleo yao kiutumishi”.**



*Baadhi ya Walimu wilayani Kahama wakiwa katika mkutano ulioongozwa na ofisi ya TSC Wilaya ya Kahama ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Geita pamoja na wadau wengine wa elimu wilayani hapo wakiwa katika mkutano na waalimu ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma iliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*



*Baadhi ya Walimu wilayani Geita wakiwa katika mkutano ulioongozwa na ofisi ya TSC Wilaya ya Geita ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika Juni 16 – 23, 2022.*

# UONGOZI WA KLABU YA MICHEZO YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC SPORTS CLUB) WAANZA MAANDALIZI KUSHIRIKI MICHEZO YA SHIMIWI 2022 MKOANI TANGA



*Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Sports Club) Ndg. Gerard Chami.*

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma**

Uongozi wa Klabu ya Michezo ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Sports Club) umekiri kuanza kwa hatua za awali ili kuweza kushiriki Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI, 2022) iliyopangwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu mkoani Tanga.

Akizungumza na SAUTI YA TSC, Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC Sports Club) Ndg. Gerard Chami alisema yeye na viongozi wenzake wa klabu baada ya kumalizika kwa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Viongozi wa SHIMIWI Taifa uliofanyika mkoani Morogoro, tayari wameanza kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa katika Mkutano Mkuu mara baada ya uchaguzi ili kuweza kushiriki katika michezo hiyo inayotarajiwa kufanyika mkoani Tanga mwaka huu 2022.

"Ni kweli baada ya Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Viongozi wa SHIMIWI Taifa uliofanyika mkoani Morogoro tayari tumeanza kutekeleza baadhi ya hatua za awali za maelekezo ya Mkutano Mkuu ikiwa ni pamoja na kushughulikia usajili wa Katiba ya Klabu, kuanzisha mchakato wa malipo ya ada ya Uanachama, Ada ya Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Ada ya Ushiriki wa Michezo hiyo, na vile muda sio rafiki tumeanza kuangalia namna bora ya kushirikisha Watumishi wa Ofisi za Tume Wilayani ambao




*Watumishi wa TSC wakiwa na bango wakati wa maandamano ya kuelekea ufunguzi wa mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika mwaka 2021 mkoani Morogoro.*

# UONGOZI WA KLABU YA MICHEZO YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC SPORTS CLUB) WAANZA MAANDALIZI KUSHIRIKI MICHEZO YA SHIMIWI 2022 MKOANI TANGA

ni wachezaji wa michezo tofauti iliyoainishwa na Shirikisho kushindaniwa mkoani Tanga mwezi Oktoba." Alisema Chami

Mwenyekiti huyo alisema moja ya hatua za awali katika kuhakikisha ushiriki wa watumishi wanamichezo kutoka Ofisi za TSC Wilaya ambazo ziko katika wilaya 139 hapa nchini ni pamoja na kuandaa fomu maalumu ya usajili wa ndani wa watumishi wanamichezo ambazo zikikamilika zitatumwa katika wilaya zote 139 ambako kuna Ofisi za Tume ili waweze kujaza na kuziwasilisha kwa ajili ya usajili wa ndani na upembuzi yakinifu wa ndani kwa namna ambayo Uongozi utaona njia sahihi na muafaka ya kufanya upembuzi wa wachezaji watakaoshiriki katika michezo hiyo mkoani Tanga.

Aidha Mwenyekiti huyo alisema vile Tume haina sura ya Muungano watumishi wa Tume watakaoshiriki ni wale watakaotoka katika wilaya 139 tu Tanzania Bara ambako Tume ina ofisi na wale ambao wana mahitaji maalumu kama ilivyoelekezwa na Mkutano Mkuu wa SHIMIWI.

Vilevile Chami alisema maandalizi ya Rasimu ya Bajeti ya Ushiriki wa Michezo hiyo umeanza huku akiitaja michezo iliyoainishwa na Shirikisho hilo kushindaniwa kuwa ni pamoja na Mpira wa Miguu, Netiboli, Kuvuta Kamba kwa wanawake na wanaume, Baiskeli kwa wanawake na wanaume, Karata kwa wanawake na wanaume, Bao kwa wanawake na wanaume, Drafti kwa wanawake na wanaume, Vishale (Darts) kwa wanaume na Riadha ambayo ndani yake kuna michezo ya kurusha tufe, kurusha kisahani, kurusha mkuki, mbio ndefu, mbio fupi, kuruka juu na kuruka chini yote kwa wanawake na wanaume.



*Watumishi wa TSC wakiwa katika maandamano ya kuelekea ufunguzi wa mashindano ya SHIMIWI mwaka 2021 mkoani Morogoro.*

Hata hivyo alieleza changamoto ya ufinyu wa bajeti na namna Uongozi unavyojitahidi kukabiliana nayo kwa kuwasiliana na wadau mbalimbali wa Tume wanaoshirikiana katika shughuli na matukio mbalimbali ili kuangalia namna wadau hao wanavyoweza kusaidia Klabu ya Tume kujiandaa vema na kushiriki katika michezo mbalimbali na mabonanza ndani na nje ya mkoa wa Dodoma ambako ndiko Makao Makuu ya Klabu.

Chami kwa niaba ya Uongozi mzima wa Klabu ya Tume alimshukuru sana Mwenyekiti wa Tume, Makamishna na Uongozi wote wa Tume kwa kuruhusu Watumishi kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo SHIMIWI kwani ridhio lao linaendana na matumizi ya fedha ambazo wangeweza kuelekeza kwenye miradi na matumizi mengine ya Tume.

Hali kadhalika alitoa pongezi nyingi kwa timu za Tembo Warriors (wenye mahitaji maalumu) na ile ya Mpira wa Miguu ya Wasichana (Serengeti Girls) kwa kulipa Taifa la Tanzania heshma kubwa baada ya kufanikiwa kutinga katika michezo ngazi ya Dunia (World Cup) katika madaraja yao.




*Watumishi wa TSC wakiwa katika maandamano ya kuelekea ufunguzi wa mashindano ya SHIMIWI mwaka 2021 mkoani Morogoro.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (upande wa kulia mwenye miwani) akiwa katika picha ya pamoja na wachezaji wa mpira wa pete wa TSC wakati wa mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika mwaka 2021 mkoani Morogoro.*



*Watumishi wa TSC wakishangilia wakati wa mashindano ya SHIMIWI yanayofanyika mwaka 2021 mkoani Morogoro.*



*Wachezaji wa mpira wa pete wa TSC (rangi ya bluu) wakicheza kwenye mashindano ya SHIMIWI mwaka 2021 mkoani Morogoro.*

# UCHAGUZI MKUU WA SHIRIKISHO LA MICHEZO YA WIZARA NA IDARA ZA SERIKALI WAFANYIKA KWA UMAHIRI MKUBWA

**Na Mwandishi wetu - Morogoro.**

WAJUMBE 70 kati ya 100 wa mkutano mkuu wa uchaguzi wamemchagua Bw. Daniel Mwalusamba kuwa Mwenyekiti wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), katika uchaguzi uliofanyika hivi karibuni kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Hoteli ya Mount Uluguru, mkoani Morogoro.

Msimamizi wa uchaguzi huo uliosimamiwa kwa umakini na uadilifu mkubwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Bw. Leonard Thadeo, alisema nafasi hiyo iliwaniwa na wanamichezo wawili, ambapo Bw. Eliud Mwaiteleke alipata kura 30; huku nafasi ya Makamu Mwenyekiti ikichukuliwa na Bw. Alquine Masubo aliyepata kura 64 na kuwashinda Bw. Kaundime Kizaba aliyepata kura 18 na Bw. Chilemba Chikawe aliyepata kura 16 kati ya 100 zilizopigwa.

Bw. Thadeo alisema kuwa



*Mwenyekiti wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Daniel Mwalusamba akila kiapo baada ya kuchaguliwa tena na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa shirikisho hilo kwa kura 70 kati ya 100 uliofanyika leo kwenye ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Mount Uluguru, mkoani Morogoro.*



*Msimamizi wa uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Leonard Thadeo (aliyenyoosha kidole) wakati akizungumza na wajumbe waliokasimiwa madaraka na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kusimamia uchaguzi huo wakiwa wanazungumza mambo mbalimbali baada ya zoezi hilo kukamilika kwenye ukumbi wa mikutano wa Hoteli ya Mounti Uluguru, mkoani Morogoro.*



*Mmoja wa wajumbe wa uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), Mohamed Ally (wapili kulia) akisimamia zoezi la kuhesabu kura za wagombea wa nafasi ya ujumbe wa kamati ya utendaji katika uchaguzi uliofanyika leo kwenye ukumbi wa Hoteli ya Mount Uluguru, mkoani Morogoro.*

# UCHAGUZI MKUU WA SHIRIKISHO LA MICHEZO YA WIZARA NA IDARA ZA SERIKALI WAFANYIKA KWA UMAHIRI MKUBWA

Bw. Alex Temba amechaguliwa kwa kura 80 kuwa Katibu Mkuu na kumshinda Bw. Mussa James aliyepata kura 20; huku nafasi ya Katibu Msaidizi akichaguliwa Bi. Mariam Kihange aliyepata kura 56 na kuwashinda Bw. Mfaume Mfaume (21), Bw. Andrew Sekimweri (14) na Bw. Mwinjuma Bwanga (7); huku Bi. Rose Makange aliyekuwa hana mshindani katika nafasi ya Mweka Hazina akishinda kwa kishindo nafasi hiyo kwa kuzoa kura zote 100.

Wajumbe wawili wa Viti Maalum Wanawake wameshinda; Bi. Itika Mwankenja kwa kura 81 na Bi. Bahati Mollel kwa kura 68, huku Bi. Assumpta Mwilanga akishindwa kwa kupata kura 37 ambazo hazikutosha; na Wajumbe watano kati ya sita wa Kamati ya Utendaji walioshinda wakiwa ni Bw. Tumsifu Mwasamale (91), Bw. William Moye (89), Bw. Apolinary Kayungi (85), Bw. Damian Manembe (83) na Bw. Mashaka Mwamage (74), huku Bw. Fidelis Choka akiangukia pua kwa kupata jumla ya kura 57 ambazo hazikutosha.

Hata hivyo, Msimamizi wa Uchaguzi Bw. Thadeo alisema wanamicbezo 21 ndio walijitokeza kuwania nafasi mbalimbali katika Shirikisho hilo, huku wapiga kura wakiwa 100, na aliwashukuru wagombea wote kwa kushiriki vyema katika hatua zote ikiwemo ya awali ya usaili, kampeni na baadaye kwenye uchaguzi bila ya kuwa na matatizo. Hali kadhalika aliwashukuru wajumbe wote na wapiga kura kwa kufuata Taratibu na Kanuni zilizowekwa na BMT na kufanikisha uchaguzi huo salama.

"Wanamichezo wameitikia wito na kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali tangu ilivyotangazwa hata kwenye usaili waliweza kufika ni 16 baada ya watano kushindwa kufika na ndio waliochujwa, na kimsingi uchaguzi ulikwenda vizuri sana maana tulipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wenzetu na pia hatujapata malalamiko kutoka kwa wagombea walioshindwa," alisema Msimamizi wa Uchaguzi huo.

Naye Mwenyekiti Mteule Bw. Daniel Mwalusamba aliwashukuru Wajumbe kwa kumchagua tena katika nafasi ya Uenyekiti kwani wameonesha imani kubwa juu yake na katika utendaji wake wa kazi na hivyo kumpa tena dhamana ya miaka minne ijayo ya kuongoza, ambapo pamoja na shukrani hizo aliahidi kwa kushirikiana na Viongozi wenzake wa Kamati ya Utendaji watahakikisha wanatekeleza maazimio yote ya Mkutano Mkuu kama yalivyoafikiwa na kupitishwa na Wajumbe.

Tume ya Utumishi wa Walimu iliwakilishwa na wajumbe watatu katika Mkutano huo akiwemo Mwenyekiti, Katibu na Mwakilishi wa TUGHE wa Klabu ya Michezo ya TSC.



*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), wakifurahia jambo wakati wa mchakato wa upigaji kura uliofanyika leo kwenye ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Mount Uluguru,, mkoani Morogoro.*



*Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI), wakifuatilia kwa makini masuala yaliyokuwa yakielezwa na msimamizi wa uchaguzi huo, Leonard Thadei (hayupo pichani) kwenye ukumbi wa mikutano wa hoteli ya Mount Uluguru,, mkoani Morogoro.*




**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania